

**Dondoo za mkuutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**  
**Tarehe 10 Machi 2007**

**Waliohudhria**

Abdallah Khatib

Elaine Baker

Juma Ali Salehe Jongo

Shukuru Hassan

**Wageni**

Mr Nyoni, AALOCOM

Bradley Schroeder, Institute for Transportation & Development Policy (ITDP) (Taasisi ya Usafirishaji na Maendeleo)

Bradley aliuliza jinsi msafara wa baiskeli ulivyokwenda, akajibiwa kuwa ulikwenda salama. Ndugu Nyoni alisema kwamba watu 200 walishiriki. Kulikuwa na mvutano kati ya baadhi ya mashirika mfano wakati wa mabadiliko ya ukumbi. CHABADA ilimudu nafasi yake vizuri kama waongozaji. Idadi kubwa ya walemvu ilishiriki na baiskeli za mikono. Tukio lilichukuliwa na Runinga ingawa walinukuu kinyume kama mashindano ya baiskeli.

Bradley alisema lilikuwa tukio zuri ingawa alidhani halikuandaliwa vizuri. Kutokana na baadhi ya vipengele kutokupangwa kwa ufasaha kwa mfano baadhi ya matumizi kama ya maji yangeweza kupatikana kwenye makampuni ya ya maji. Alisema lilikwa lilikuwa tukio lililotumia gharama kubwa (\$ 600 ) kwa mtazamo wa ITDP. alikiambia kikundi kuwa Ghana msafara kama huo ulifanywa kwa gharama za ufadhilli wa makampuni makubwa . Elaine alieleza kuwa kupata ufadhilli mkubwa inamaanisha kuwa kama kutangaza makampuni hayo badala ya kutangaza matukio ya upandaji baiskeli. Bradley alikubali kuwa ni kweli lakini alisema kwa upande mwengine inasaidia kufanikisha tukio na kulifanya lijulikane zaidi.

Bradley alieleza kuwa AALOCOM haina mpango wa kuwa a madaraka kwenye shirika mbeleni ila Ndugu Nyoni, ambaye ameajiriwa na mradi wa baiskeli wa California, atawezu kushiriki kwenye shirika.

Elaine alisema kuwa UWABA ingependa kuandaa msafara kama tukio la mwaka. Ila akasema kuandaa inahitaji kuchukua muda mwangi wa watu wenye uwezo na ujasiri wa kuongea na viongozi wa serikali. Polise na wafadhili pamoja na muda wa kusambaza barua ,kuomba mikutano n.k AALOCOM iliongoza katika maeneo ya msafara uliopita wakati UWABA ilikuwa ikichapa na kusambaza vipeperushi, kuweka mabango na kukusanya washiriki. Hivyo aliomba AAЛОOM itoe wafanyakazi kwa muda wote na/au watu wa ziada kutoka UWABA /AALOCOM/CHABADA wapewe fedha za kujikimu ili kufanya kazi wakati wote wa tukio kwa miezi miwili

Bradley alisema ITDP itahiari kusaidia tukio kwa kutuwezesha kuwasiliana na viongozi wa serikali na kutusaidia kuvutia ukusanyaji wa fedha.

Ilikubalika kwa maendeleo UWABA na AAALOCOM zikutane na kufanya kazi mipango ya msafara ujao na jinsi shughuli za shirika zitakavyofanywa, vitu, gharama zitakazohitajika n.k. kasha zitumwe kwa Bradley kwa barua pepe kwa ushauri wake na msaada.

Kulikuwa na mjadala kuhusu mradi wa mabasi yaendayo kasi, itakuwa faida kubwa kwa wapanda balskeli kutohana na ukuaji wa naul za mabasi na upungufu wa watoa huduma ya mabasi katika sehemu fupi fupi na za ndanindani.

Kulikuwa na mjadala pia kuhusu harakati za usafishaji jiji kwa kuwaondoa wafanyabiashara ndongondogo. Hii iliachia njia katika barabara kuu kwa wapanda balskeli lakini pia hilo lilifanywa kikatili bila kuhusisha wahusika na vuruga maisha ya watu waliokuwa wanafanya biashara wenyewe vioski mbali na barabara kuu ambapo havikuwa vinasababisha msongamano.

Ilitajwa kuwa mkuu wa TANROADS ni Mghana na Bradley angeweza kuongea nae kwavile aliishi huko kwa muda na kwa muunganisho wa msafara, labda Bradley atawenza kuonana nae.

Ilikubalika kuwaa AAALOCOM na UWABA zikutane tarehe 31 machi saa 4 asubuhi Msasani baa kupanga msafara wa balskeli ujao.